# MASIHA WETU NJOO

F . A . Nyundo




**Dom I:**

1. Ee Bwana nakuinulia nafsi yangu,ee Mungu wangu / nimekutumaini wewe nisiaibike, adui zangu wasifurahi kwa kunishinda.
2. Naam, wakungojao hawataaibika hata mmoja / wataaibika watendao uhaini bila sababu.
3. Ee Bwana unijulishe njia zako / unifundishe mapito yako.

**Dom II:**

1. Ee Bwana usikie kuomba kwangu / kilio changu kikufikie.
2. Usinifiche uso wakati wa shida / unitegee sikio lako, siku niitapo unijibu upesi.
3. Maana siku zangu zimetoweka kama moshi / na mifupa yangu imeteketea kama kinga.

**Dom III:**

1. Furahi katika Bwana siku zote / tena nasema furahini.
2. Upole wenu ujulikane kwa watu wote / Maana bwana yukaribu.
3. Msijisumbue kwa neno lolote / bali kwa kila neno kwa kusali na kuomba pamoja na kushukuru.

**Dom IV:**

1. Dondokeni enyi mbingu toka juu / mawingu na ya mmwage mwenye haki.
2. Nchi na ifunuke ili kumtoa mwokozi / nayo itoe haki ikamee pamoja.
3. Bwana umeiridhia nchi yako / umewarejeza mateka wa Yakobo.